JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", MTWARA
Nambari ya Simu: 023-2333944
Fax Na: 023-2334098

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula

S.L.P. 520
**MTWARA**

Unapojibu Tafadhali taja:-

**Kumbukumbu Na:-CG.140/47**

**Tarehe:** 20/08/2025

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI ZA KUJITOLEA

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mtwara – Ligula anakaribisha maombi ya kazi za kuijitolea kwa kada mbalimbali kama ilivyoahinishwa hapo chini:-

### 1. AFISA HABARI DARAJA LA II – NAFASI 1

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Shahada ya Kwanza au Stashahada ya Juu ya Uandishi wa Habari au sifa inayolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kukusanya na kuandika habari.
ii. Kupiga picha.
iii. Kuandaa picha za maonyesho.
iv. Kuandaa majarida na mabango (Posters).
v. Kukusanya takwimu mbalimbali.
vi. Kuandaa majarida na vipeperushi.
vii. Kuhifadhi picha na kuhudumia maktaba na marejeo.

### 2. FUNDI SANIFU VIFAA TIBA DARAJA LA II – (NAFASI 1)

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye Stashahada ya kawaida ya ufundi (Full Technician Certificate) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kufanya Matengenezo ya Vifaa vya huduma za tiba katika Hospitali za Wilaya
ii. Kutunza kumbukumbu za kazi za kila siku
iii. Kuinziza vifaa na vipuli vya kutengenezea Vifaa Tiba ngazi ya Wilaya
iv. Kutunza Vifaa Tiba na vipuli
v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wakazi

3. **DATA ENTRY (NAFASI 5)**

**SIFA ZA KUINGILIA**

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha IV/VI, aliehitimu angalau stashahada katika fani yeyote kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali

**KAZI NA MAJUKUMU.**

i. Kukusanya fomu zote za BIMA Hospitalini
ii. Kuchakata madai ya BIMA zote (kuingiza madai kwenye mfumo)
iii. Kuchakata makato ya BIMA zote.
iv. Kupokea na kuwasajili wagonjwa
v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

4. **DEREVA (NAFASI 01)**

**SIFA ZA KUINGILIA**

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha IV,awe na leseni iliyolipiwa daraja E au C1 , Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji gari inayotolewa na Chuo cha mafunzo ufundi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali, awe na uzoefu wa miaka 3 bila kusababisha ajali,awe na cheti cha mjaribio ya ufundi Daraja la II

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari "Log Book"
vi. Kufanya usafi wa gari
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

**5. MORTUARY ATTENDANT (NAFASI 1)**

**SIFA ZA KUINGILIA**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye cheti na uzoefu wa kazi za uhudumu katika chumba cha kuhifadhi maiti kwa muda usiopungua miaka miwili.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kufanya usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti
ii. Kupokea kuosha na kutunza maiti
iii. Kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi

**NB: MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania
ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa
iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detail CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika
iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika

Viambatanisho hivyo vibanwe sawasawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea:-

- Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI kwa waliofika kidato cha VI
- Vyeti vya kitaaluma (Professional certificate from respective boards)
- Leseni ya Uuguzi na Ukunga
- Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma

v. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

vi. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **04/09/2025** saa **9:30 Alasili**

vii. Aidha atakaewasilisha barua yake kwa njia ya mkono ahakikishe anasaini kitabu maalumu cha kupokea barua hizi Masijala

viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na yatumwe kupitia anuani ifuatayo:-

Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara,
S.L.P 520,
**MTWARA**

LIGULA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL
P.O. Box 520
MTWARA